**HOTUBA YA DKT. AGNES L. KIJAZI, MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA HALI YA HEWA DUNIANI TAREHE 23 MACHI 2017**

Kila tarehe 23 Machi, Tanzania huungana na nchi wanachama wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) na jumuiya ya hali ya hewa kukumbuka na kusherehekea kuanzishwa kwa Shirika la Hali ya Hewa Duniani. Shirika hili lilianzishwa miaka 67 iliyopita.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) inatekeleza makubaliano, miongozo, kanuni na taratibu za Shirika la Hali ya Hewa Dunuani (WMO) kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kuadhimisha Siku ya Hali ya Hewa Duniani (WMD) TMA inachukua fursa hiyo kwa kuelezea faida za matumizi ya huduma za hali ya hewa nchini na mafanikio ya TMA.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania iliundwa mwaka 1999 kama wakala wa Serikali kwa sheria Na. 30 ya mwaka 1997. Miongoni mwa majukumu ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ni kufanya uangazi, kukusanya na kuhifadhi takwimu za hali ya hewa, uchambuzi, utoaji na usambazaji wa taarifa za hali ya hewa katika Jamuhuri ya Muungno wa Tanzania. Mamlaka pia hutoa huduma za hali ya hewa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya usafiri wa anga, hushiriki katika kubadilishana kimataifa takwimu na taarifa za hali ya hewa kwa ajili ya usalama wa watu na mali zao. Aidha, Mamlaka hushiriki katika kutekeleza majukumu mbalimbali kwa kuzingatia makubaliano ya kimataifa kama vile makubaliano kupitia Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO).

Maadhimisho ya Siku ya Hali ya Hewa Dunani (WMD) huambatana na kaulimbiu, ambapo kaulimbiu ya mwaka huu ni “***Tuyaelewe Mawingu na umuhimu wake - Understanding Clouds***"; Kaulimbiu hii inaeleza mchango wa mawingu katika kutoa utabiri na tahadhari. Mawingu yana mchango mkubwa katika mzunguko na mtawanyiko wa rasilimali za maji pamoja na joto duniani kote.

Kaulimbiu ya mwaka huu imechaguliwa katika kuhitimisha kilele cha toleo jipya la Atlasi ya Kimataifa ya Mawingu ya Kidigitali “***new digital International Cloud Atlas”.*** Toleo hili jipya la Atlasi linazinduliwa rasmi leo siku ya maadhimisho tarehe 23 Machi, 2017. Mawingu huathiri hali ya hewa kwa njia mbalimbali na yanaweza kutambuliwa kwa kuangalia muundo na muonekano wake angani. Majina mengi ya mawingu yanaviambishi vya kilatini vinapounganishwa hutoa

mwelekeo wa tabia ya wingu. Majina hayo ni pamoja na***;*** (i) ***Stratasi/strato*** **-** yanaonekana tambalale, yenye tabaka/safu na manyororo ‘‘flat, layered and smooth)’’**;** ***(ii) Kumulas/kumulo*** **-** hujikusanya na yenye miinuko ‘‘heaped up, puffy’’; (iii) ***Sirras/sirro*** **-** hufanana na manyoya au moshi (feathery, wispy); (iv) ***Nimbusi/nimbo – mazito meusi na hutoa mvua nyingi ‘‘rain-bearing’’, (v) Alto – huwepo kati ya mawingu ya juu na chini ‘‘mid-level’’.***

Baadhi ya mawingu husababisha aina mbali mbali za mvua (mfano rasharasha, theluji au barafu) na yanahusika katika kubadili joto la eneo husika duniani. Mathalani, mawingu yakiwa chini, karibu na ardhi na yametanda husababisha baridi, wakati yakiwa juu angani na yametanda husababisha joto kuongezeka. Halikadhalika, mawingu yanaporuhusu mionzi ya joto kutoka kwenye uso wa duniani kwenda angani yanapelekea joto kuwepo katika uwiano sawia katika uso wa dunia hivyo kuweka hali ya joto katika kiwango kinachohitajika. Hata hivyo, utafiti wa hivi karibuni unaonesha kuwa athari za mawingu katika hali ya hewa zinatarajiwa kubadilika kutokana na ongezeko la joto duniani.

Tunaposherehekea siku ya hali ya hewa duniani (WMD), TMA inaendelea kuwashauri watumiaji wote wa huduma za hali ya hewa kuhakikisha kwamba wanadumisha mawasiliano ya karibu na TMA ili kuboresha huduma mbalimbali katika sekta zao za kiuchumi kwa ustawi wa jamii nchini. Kupitia vifaa vya uangazi wa hali ya hewa TMA daima imekuwa ikitoa huduma muhimu katika sekta za kijamii na kiuchumi kama vile kilimo, usafiri wa anga, maji, nishati, afya, ujenzi, utalii na utafiti katika Taasisi za elimu ya juu. Halikadhalika Mamlaka inajukumu la kuhakikisha sayansi ya hali ya hewa inaendelezwa hapa nchini. Katika kutimiza lengo hili, wataalam wa Mamlaka wameendelea kufundisha na kufanya utafiti wa hali ya hewa na mazingira kwa kushirikiana na taasisi za elimu ya juu ndani na nje ya nchi.

Taarifa za hali ya hewa hupatikana katika njia mbalimbali kama vile takwimu au utabiri katika vipindi tofauti ikijumuisha utabiri wa kila siku, siku kumi, mwezi na msimu. Taarifa za hali ya hewa hutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwani wadau hutumia taarifa hizi katika maamuzi. Kitovu cha masuala yote katika Mamlaka ni kuridhika kwa wadau kutokana na huduma zitolewazo na Mamlaka, Mamlaka imeendelea kukidhi mahitaji ya wadau kama moja ya malengo yake kupitia mchango unaotolewa na Serikali pamoja na washirika wa maendeleo.

Tunaposherekea siku ya hali ya hewa Duniani (WMD) Mamlaka inaendelea kuuhamasisha umma kwa ujumla kutembelea vituo vya hali ya hewa vilivyoko katika maeneo mbalimbali nchini ili waweze kufahamu huduma zinazotolewa na Mamlaka ili waweze kuzitumia katika shughuli zao za kila siku kwa maendeleo endelevu. Wakati wa kutembelea vituo hivyo, wadau watapata fursa ya kujifunza sayansi ya hali ya hewa ikiwemo namna mawingu yanavyotumika katika utabiri wa kila siku.

Mwisho nawatakia wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sherehe njema za siku ya hali ya hewa duniani. “Tuyaelewe Mawingu na umuhimu wake”.